


SHIRIKA LA MAENDELEO YA PETROLI TANZANIA




**TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA UJENZI WA MIUNDOMBINU YA
GESI ASILIA KUTOKA MADIMBA – MTWARA, SONGO SONGO –
LINDI NA PWANI HADI DAR ES SALAAM**

MACHI, 2015

UTANGULIZI

1. Shughuli za utafutaji mafuta na gesi asilia nchini zilianza miaka ya 1950 kupitia Kampuni ya Agip kutoka Italia. Licha ya shughuli hizo kuanza miaka ya 1950, Kampuni ya Agip ilifanya ugunduzi wa kwanza katika **Kisiwa cha Songo Songo** (Lindi) mwaka 1974 ambao ulifuatiwa na ugunduzi mwingine katika eneo la Mnazi Bay (Mtwara) mwaka 1982. Hata hivyo, gesi asilia hiyo haikuendelezwa kwa kuwa ilionekana haina manufaa ya kiuchumi (*uneconomical*) kwa wakati huo. Baada ya ugunduzi huo, TPDC iliendelea kufanya utafiti ikiwa ni pamoja na kuchimba Visima mbalimbali kwa ajili ya kuthibitisha kiasi cha gesi asilia kilichopo katika maeneo ambako gesi asilia iliyogunduliwa. Hadi Novemba, 2014 kiasi cha gesi asilia kilichogunduliwa nchini ni **futi za ujazo triloni 53.28** (53.28TCF) kama inavyooneshwa kwenye Kielelezo Na.1.

Kielelezo Na.1: Kiasi cha Gesi Asilia Kilichogunduliwa



2. Ili kuhakikisha kuwa nchi **inanufaika na rasilimali ya gesi asilia iliyogunduliwa nchini**, Serikali kupitia TPDC inakamilisha utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa mitambo ya kusafisha gesi asilia katika maeneo ya Madimba (Mtwara) na Songo Songo (Lindi) pamoja na Bomba la kusafirisha gesi asilia hiyo kutoka Mtwara, kupitia Somanga Fungu (Lindi), Pwani hadi Dar es Salaam. Lengo la Serikali ni kuhakikisha kuwa gesi asilia mbali na matumizi mengine, itumike katika kuzalisha umeme

ambao kwa sasa unazalishwa kwa kutumia **mafuta ambayo ni ghali**. Kwa kiasi kikubwa, mradi huo unatekelezwa kwa fedha za mkopo wa masharti nafuu kutoka Benki ya Exim ya China.

Pamoja na mambo mengine, taarifa hii inaelezea hatua za **utekelezaji wa mradi huo**.

HISTORIA YA MIUNDOMBINU YA GESI ASILIA NCHINI


Kwa takriban miaka ishirini **(20) tangu kugunduliwa kwa gesi asilia nchini**, Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali iliendelea kufanya tafiti za namna ya kutumia rasilimali hiyo. Utafiti wa mwisho ulikamilika mwaka 1991 ambapo mradi wa ujenzi wa mitambo ya kusafisha gesi asilia Kisiwani Songo Songo pamoja na Bomba la kusafirisha gesi asilia hiyo mpaka Dar es Salaam ulibuniwa.

3. Ili kutekeleza mradi huo, **Serikali ilikopa fedha kutoka Benki ya Dunia na Benki ya Rasilimali ya Ulaya (EIB)**. Utekelezaji wa mradi wa Songo Songo ulikuwa na malengo yafuatayo:

- a) Kupunguza utegemezi wa umeme unaozalishwa kwa kutumia maji (*hydro power*) ambao unaathiriwa na mabadiliko ya tabianchi kama ukame;
- b) Kupunguza matumizi ya fedha za kigeni zinazotumika kuagiza mafuta kutoka nje kwa ajili kuzalisha umeme;
- c) Kushirikisha Sekta Binafsi katika Sekta ya Nishati; na
- d) Kuvutia wawekezaji katika shughuli za utafutaji mafuta na gesi asilia nchini.

4. Ili kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa mradi huo, ilishauriwa kuwa Serikali itekeleze mradi huo kwa njia ya ubia na Sekta Binafsi na kwamba chombo maalum (*a Special Purpose Vehicle*) kiundwe ili kutekeleza na kusimamia mradi huo, hivyo Kampuni ya Songas ikaanzishwa. **Kielelezo Na. 2** kinaonesha muundo wa utekelezaji wa mradi wa Songo Songo.

Kielelezo Na. 2: Muundo wa Mradi wa Songo Songo



5. Ili kufanikisha utekelezaji wa mradi huo, Songas ilikabidhiwa **visima Na. 3,4,5,7 na 9** vilivyochimbwa na Serikali kupitia TPDC katika eneo la Songo Songo ili kuviendesha. Aidha, mwaka 2001, Serikali iliingia Mkataba wa Uzalishaji na Ugawanaji mapato (PSA) na Kampuni ya PanAfrican Energy Tanzania Limited (PAET) kwa ajili ya kuendeleza eneo la Songo Songo. Kupitia PSA hiyo ya mwaka 2001, Songas iliikabidhi PAET jukumu la kuendesha na kusimamia visima hivyo kwa kuingia nao Mkataba wa Uendeshaji (*Operatorship Agreement*).

6. Mradi huo ulichukua takriban miaka mitatu (3) na ulikamilika **mwezi Julai, 2004** ukihusisha ujenzi wa mitambo ya kusafisha gesi asilia kiasi cha futi za ujazo milioni 70 kwa siku (*70mmscfd*) na Bomba la kusafirisha gesi asilia la inchi 16 lenye urefu wa kilomita 247 kutoka Songo Songo (Lindi) hadi Dar es Salaam. **Gharama za mradi huo zilikuwa takriban Dola za Marekani 225,347,062.** Kukamilika kwa mradi huo kumeleta unafuu mkubwa katika shughuli za uzalishaji umeme kwani **takriban megawati 300** zinazalishwa kwa kutumia gesi asilia kila siku. Aidha, gesi asilia hiyo inatumika kwenye viwanda 37, magari 60, nyumba 70, hoteli 1 na taasisi 2 (Gereza la Keko na Mgulani JKT).

7. Mnamo mwaka 2006, **Kampuni ya Artumas pia ilifanikiwa kuendeleza** Kitalu cha Mnazi Bay kwa kufufua Kisima Na. **1 kilichogunduliwa mwaka 1982 na Kampuni ya Agip** na kuongeza

visima vingine vitatu. Uendelezaji wa Kitalu hicho uliambatana na ujenzi wa mtambo mdogo wa kusafisha gesi asilia wenye uwezo wa kusafisha futi za ujazo milioni 10 kwa siku (10mmscfd) na ujenzi wa Bomba la gesi asilia la inchi 8 lenye urefu wa kilomita 27 kutoka Mnazi Bay hadi Mtwara Mjini. Kiasi cha futi za ujazo milioni 2.1 kinatumika kuzalisha umeme kwenye mitambo ya TANESCO iliyoko Mkoani Mtwara na inayohudumia Mikoa ya Mtwara na Lindi. Mradi huo uligharimu kiasi cha **Dola za Marekani 47,590,824.**

UPANUZI WA MIUNDOMBINU

8. Miaka mitatu tangu kuzinduliwa kwa miundombinu ya Songo Songo, mahitaji ya gesi asilia nchini yaliongezeka kwa kasi kubwa na kusababisha **miundombinu hiyo kushindwa kuhimili ongezeko hilo.** Ili kukabiliana na changamoto hiyo kwa kipindi cha mpito, Songas ililazimika kurekebisha valvu (*Thomson Valve*) ili **kuongeza uwezo wa mtambo wa kusafisha gesi asilia kutoka futi za ujazo milioni 70 hadi futi za ujazo milioni 110.**

9. Kwa mujibu wa mikataba iliyoingiwa mwaka 2001, Songas ilipewa **nafasi ya kwanza** kuwekeza kwenye miundombinu ya kusambaza gesi asilia kila fursa hiyo inapojitokeza. Ili kuongeza upatikanaji wa gesi asilia nchini juhudi mbalimbali zilifanyika zikiwemo:

a) Upanuzi wa miundombinu: Mradi ulibuniwa na Songas lakini **ukashindwa kutekelezwa** ilipofika mwaka 2008;

b) Upanuzi wa miundombinu: Mradi ulibuniwa na Songas pamoja na PAET ili kuongeza futi za ujazo milioni 35 kwa siku. Mradi huo pia **ulishindwa kutekelezwa;**

c) Mradi wa Rak Gas: Kampuni hiyo ilikusudia kujenga mitambo ya kusafisha gesi asilia na Bomba kutoka Mtwara hadi Mombasa. **Mradi huu pia haukufanikiwa.**


10. Baada ya Kampuni za Songas na PAET kupeleka pendekezo la kupanua miundombinu ya gesi asilia, EWURA ilikataa pendekezo hilo kwa maelezo kwamba gharama za upanuzi ni kubwa kuliko kiasi cha gesi asilia kitakachoongezeka. Kampuni za Songas na PAET zilipendekeza kutumia takriban **Dola za Marekani milioni 121** ili kuongeza **futi za ujazo milioni 35 kwa siku.**

11. Ili kukabiliana na changamoto ya upungufu wa miundombinu ya gesi asilia nchini na Songas kushindwa kutimiza majukumu yake, **Serikali iliamua kuanzisha mchakato wa kutafuta fedha za kuongeza miundombinu hiyo.**

UJENZI WA MIUNDOMBINU MIPYA YA GESI ASILIA INAYOMILKIWA NA SERIKALI

12. Mradi wa miundombinu ya gesi asilia unahusisha ujenzi wa mitambo ya kusafisha gesi asilia Madimba (Mtwara) pamoja na Songo Songo (Lindi) na Bomba la kusafirisha gesi asilia kutoka Mtwara, Lindi na Pwani hadi Dar es Salaam. Katika eneo la Madimba mitambo mitatu (3) yenye uwezo wa kusafisha futi za ujazo milioni 70 kila mmoja kwa siku inajengwa. Mitambo mingine miwili (2) yenye uwezo wa kusafisha futi za ujazo milioni 70 kwa kila mtambo kwa siku inajengwa eneo la Songo Songo.


13. Mitambo ya Madimba (Mtwara) itasafisha gesi asilia kutoka eneo la Mnazi Bay, Ntorya na Bahari ya kina kirefu. Mitambo ya Songo Songo (Lindi) itasafisha gesi asilia kutoka eneo la Songo Songo, Kiliwani na Bahari ya kina kirefu. **Kielelezo Na.3** kinaonesha mpangilio wa miundombinu ya gesi asilia pamoja na baadhi ya mitambo ya kuzalisha umeme. **Miundombinu hii ya gesi asilia itamilikiwa na Serikali kwa asilimia mia moja.**



Kielelezo Na. 3: Mpangilio wa Miundombinu ya Gesi Asilia

14. Bomba la kusafirisha gesi asilia linaanzia Madimba (Mtwara) na kuungana na Bomba linaloanzia Songo Songo katika eneo la Somanga Fungu (Lindi) kupitia Pwani hadi Dar es Salaam (**Kielelezo Na.4**). Ujenzi wa Bomba hilo una vipengele vifuatavyo:

- a) Bomba lenye kipenyo cha inchi 36 na urefu wa kilomita 290, kutoka Madimba hadi Somanga Fungu;
- b) Bomba lenye kipenyo cha inchi 36 na urefu wa kilometa 197, kutoka Somanga Fungu hadi Kinyerezi - Dar es Salaam;



KieKielelezo Na.4: Mchoro wa Bomba la Gesi

- c) Bomba lenye kipenyo cha inchi 24 na urefu wa kilometa 25; kutoka Kisiwani Songo Songo kupitia chini ya Bahari na kuungana na Bomba litokalo Mtwara katika eneo la Somanga Fungu; na
- d) Bomba lenye kipenyo cha inchi 16 na urefu wa kilometa 30, kutoka Kinyerezi hadi Tegeta.

15. Bomba lililojengwa lina uwezo wa kusafirisha gesi asilia futi za **ujazo milioni 784 kwa siku** na kufikia futi za **ujazo milioni 1002**

kwa siku ikiwa *Compressor* itaongezwa. Aidha, Bomba hilo limewekewa matoleo ya kuchukulia gesi asilia (*take off valves*) katika miji ya **Mtwara, Lindi, Kilwa, Somanga Fungu na Mkuranga** ili kuhakikisha kuwa Miji hiyo inapata fursa ya kupata gesi asilia.

16. Matoleo hayo yatatumika kupeleka gesi asilia kwenye maeneo ya viwanda, majumbani, mitambo ya kuzalisha umeme pamoja na matumizi mengine yatakayojitokeza. Pamoja na matoleo hayo Bomba hilo limewekewa maeneo ya kuweza kupokea gesi asilia (*tie in valves*) kutoka maeneo ambako gesi asilia imegunduliwa kama vile Mkuranga, Ntorya na kutoka kwenye Bahari ya kina kirefu.

GHARAMA ZA MRADI

17. Gharama za mradi ni **Dola za Marekani 1,225,327,000**. Kati ya fedha hizo Benki ya Exim ya China imechangia asilimia 95 na Serikali ya Tanzania asilimia 5. Kiasi hicho cha fedha kinatumika kugharamia maeneo yafuatayo:

- a) Mtambo wa kusafisha gesi asilia wa Songo Songo **Dola za Marekani 151,735,000;**
- b) Mtambo wa Kusafisha gesi asilia wa Mnazi Bay **Dola za Marekani 197,877,000;**
- c) Bomba la kusafirisha gesi asilia **Dola za Marekani 875,715,000.**

18. GHARAMA ZA UJENZI WA MIUNDOMBINU YA GESI ASILIA NCHINI NI ZA CHINI UKILINGANISHA NA MIRADI MINGINE YA AINA HIYO DUNIANI. Kwa mfano, taarifa iliyotolewa na Interstate Natural Gas Association of America (INGAA) ya Machi 2014 inaainisha kuwa wastani wa gharama za ujenzi wa Bomba la gesi asilia kwa mwaka 2011 zilikuwa ni **Dola za Marekani 94,000 kwa inchi-mile** sawa na **Dola za Marekani 58,421.4 kwa inchi-km**. Kutokana na taarifa hii, ujenzi wa Bomba la Tanzania la inchi 36 lenye urefu wa kilomita 487 ungegharimu wastani wa **Dola za Marekani 1,024,243,984.8 bila kujumuisha Bomba la majini na vituo vya kusafisha gesi vya Madimba na Songo Songo**. Bomba la Tanzania limejengwa kwa kiwango cha asilimia 14.5 chini ya kiwango cha wastani wa gharama za kimataifa.

19. Mifano mingine ya gharama za ujenzi wa Mabomba ya kusafirisha gesi asilia yanayoendelea kujengwa au yaliyojengwa hivi karibuni ni kama inavyooneshwa kwenye jedwali lifuatalo:

Mahali linapojengwa/ lilipojengwa	Kipenyo (Inchi)	Urefu (km)	Gharama (Bilion USD)	USD (Milioni)/ km
Bomba la nchi kavu, kutoka Iran hadi Pakistan (2011)	42	785	1.5	1.9
Nyhamna, Norway mpaka Easington, Uingereza-Main portion offshore (2009)	44	1,200	12	1.6
The OPAL, Germany's, supply security for Germany and Europe (2009)	55	470	1.4	2.98
Wastani kwa Bomba la Tanzania ¹		542	0.88	1.62

20. Kwa upande wa majimbo ya Marekani ambapo kazi nyingi zinafanywa na Kampuni za ndani kwa kutumia vifaa vinavyozalishwa na viwanda vya Marekani. Gharama za Ujenzi wa Mabomba ya gesi asilia iliyotekelezwa kati ya mwaka 2005 hadi 2006 nchini Marekani ni kama ifuatavyo;

¹ Wastani kwa sababu kuna bomba la majini (Urefu 25 km, Kipenyo Inchi 24), nchi kavu (Urefu 487kmm, Kipenyo Inchi 36) na nchi kavu (Urefu 30 km, Kipenyo Inchi 16)

Kipenyo	Jimbo	Urefu	Urefu	Gharama ya Ujenzi	Wastani
in		mile	km	US\$	milioni US\$/km
36	Louisiana	3	4.8	10,359,476	2.2
36	Washington	11.89	19.024	57,057,798	3.0
36	Louisiana	12	19.2	31,070,508	1.6
36	Washington	22.43	35.888	70,976,850	2.0
36	Washington	22.5	36	84,782,091	2.4
36	Texas	25	40	61,918,000	1.5
36	Washington	26.68	42.688	82,596,091	1.9
36	Texas	27.07	43.312	62,582,000	1.4
36	Maryland	47	75.2	159,178,294	2.1
36	Texas-Louisiana	70	112	206,523,594	1.8
36	Colorado	136	217.6	193,747,000	0.9
36	Texas	108	172.8	280,595,710	1.6

Angalizo 1: 1 mile = 1.609 km

21. Kutokana na ulinganisho wa gharama za ujenzi wa miundombinu ya gesi asilia duniani **ni dhahiri kuwa gharama za ujenzi wa miundombinu ya gesi asilia Tanzania ni ya bei nafuu.**

UTEKELEZAJI WA MRADI

KAZI ZILIZOKAMILIKA KATIKA UJENZI WA BOMBA LA GESI ASILIA

22. Mkandarasi wa ujenzi wa Bomba la gesi asilia alianza kazi ya kuunganisha mabomba (*pipe welding*) **tarehe 26 Agosti, 2013** kwa kupitia vikosi sita (6) vya kuunganisha mabomba kwa maeneo ya ujenzi ya nchi kavu. Hadi kufikia Februari 2015, Mkandarasi ameteteleza kazi kama ifuatavyo:

- a) Hatua ya awali ya usanifu wa mradi huu (*Front End Engineering Design – FEED*) imekamilika kwa asilimia 100;
- b) *Hazard Operatibility Studies (HAZOP)* imekamilika kwa asilimia 100;

- c) Ununuzi na upelekaji wa vifaa sehemu ya kazi imekamilika kwa asilimia 99.29;
- d) Uunganishaji wa mabomba umekamilika kwa asilimia 100;



- e) Kufanya ukaguzi wa kina wa kitaalam kwenye eneo la Bomba palipounganishwa (*non destructive testing –NDT*) kumekamilika kwa asilimia 100;
- f) Kazi ya kuvusha Bomba la gesi asilia chini ya Mto Rufiji kwa *Horizontal Directional Drilling (HDD)* imekamilika kwa asilimia 100 ikiwa ni pamoja na kupitisha mkongo wa mawasiliano (*FOC*);
- g) Kulifukia Bomba la gesi asilia pamoja na mkongo wa mawasiliano (*Backfilling*) kumekamilika kwa asilimia 99.1;
- h) Bomba la gesi asilia chini ya Bahari kutokea Somanga Fungu hadi Songo Songo kilomita zipatazo 30 limekamilika kwa asilimia 100; na
- i) Ujenzi wa *Valve Stations* unaendelea kwa valve zote 16 na ujenzi wa vituo vya kupokelea gesi asilia eneo la Somanga Fungu umefikia asilimia 94, Kinyerezi Dar es Salaam umefikia asilimia 97 na Tegeta umefikia asilimia 97.

Jedwali Na. 1: Muhtasari wa Utekelezaji wa Mradi kwa Mkandarasi wa Ujenzi wa Bomba la gesi asilia hadi Februari, 2015

Kazi kwa Mgawanyo	Uzito wa kila kazi kwa %	Mpango %	Halisi %	Utofauti %
Maandalizi ya Mradi na Menejimenti yake	14.68	100.00	100.00	0.00
Usanifu	14.36	100.00	100.00	0.00
Manunuzi	25.37	100.00	99.29	(0.71)
Ujenzi	45.59	98.29	97.79	(0.50)
Jumla yote	100.00	99.22	98.81	(0.41)

Kazi zilizokamilika katika Ujenzi wa Mitambo ya Kusafisha Gesi Asilia

23. Mkandarasi wa ujenzi wa mitambo ya kusafisha gesi (*CPE*) alianza ujenzi wa kambi za kuishi wafanyakazi na maandalizi ya eneo la ujenzi wa mitambo ya kusafisha gesi **mwezi Septemba 2013**. Hadi Januari, 2015 Mkandarasi huyo amekamilisha kazi zifuatazo:

a)Ujenzi wa nyumba za kuishi wafanyakazi sehemu za Madimba (Mtwara) na Songo Songo (Lindi) umefikia asilimia 100;



- b)Ujenzi wa eneo la kusimika mitambo (*civil works for processing plants*) umekamilika kwa asilimia 95 kwa Madimba na asilimia 88 kwa Songo Songo;
- c)Ujenzi wa Bomba la kusafirisha gesi asilia isiyosafishwa (*raw gas*) kwa upande wa Baharini kutokea Msimbati kilometa 4.78 umekamilika kwa asilimia 100;
- d)Usimikaji wa mitambo ya kusafisha gesi Madimba na Songo Songo umefikia asilimia 99;



- e)Ununuzi wa vifaa vya ujenzi wa mradi umekamilika kwa asilimia 100; na
- f) Uchimbaji wa visima vya maji yatakayotumika kwa ajili ya mitambo na wananchi wa maeneo ya jirani umekamilika kwa asilimia 100.

Jedwali Na. 2: Maendeleo ya Mradi kwa Mkandarasi wa Ujenzi wa Mitambo ya kusafisha gesi asilia hadi Februari, 2015 ni kama ifuatavyo:

Kazi kwa Mgawanyo	Uzito wa kila kazi kwa %	Mpango %	Halisi %	Utofauti %
Usanifu wa Awali	2.78	100.00	100.00	0.00
Usanifu wa kina	4.64	100.00	100.00	0.00
Manunuzi	57.08	100.00	100.00	0.00
Ujenzi	35.50	90.01	82.97	(7.04)
Jumla	100.00	96.45	93.95	(2.50)

KAZI ZINAZOENDELEA KUFANYIKA

24. Kazi zilizobaki kwa mradi kukamilika ni zifuatazo:

- a) Kukamilisha usimikaji wa mitambo ya kusafisha gesi asilia
- b) Kukamilisha ujenzi wa *Valve Stations* 16
- c) Ujenzi wa vituo vya kupokelea gesi asilia Mtwara, Somanga Fungu Kilwa, Kinyerezi na Tegeta Dar es Salaam
- d) Kukamilisha kazi ya kufanya majaribio ya mgandamizo mkubwa wa maji kwenye Bomba (*Hydrostatic pressure test*) maeneo mbalimbali katika Bomba ambapo kilometa 432 zimekamilika.
- e) Udhibiti wa ubora kwa kila hatua katika ujenzi unaoendelea;
- f) Kukamilisha uwekaji Mkongo wa Mawasiliano (*FOC*) kwenye njia ya Bomba
- g) Kumalizia ujenzi wa misingi (Civil work) ya mitambo ya kusafisha gesi asilia eneo la Madimba (Mtwara) na Songo Songo (Lindi);
- h) Kuelimisha wananchi juu ya mradi kwa makundi mbalimbali ya wananchi;
- i) Usanifu na michoro ya kuunganisha wateja wa gesi asilia wakiwemo Dangote, Meiz, Mitambo ya umeme ya Kinyerezi, Ubungo na Tegeta; na
- j) Kuendelea na maandalizi ya majaribio ya Bomba la gesi asilia na mitambo ya kusafisha gesi asilia (*Pre-commissioning and commissioning preparations*).

MANUFAA YANAYOTOKANA NA UJENZI WA MIUNDOMBINU YA GESI ASILIA

25. Utekelezaji wa mradi huu utaleta manufaa makubwa kwa Taifa letu na wananchi wake yakiwemo:

- a) **Umeme wa Uhakika na wa Bei Nafuu:** Utekelezaji wa mradi huu utaiwezesha nchi yetu kupata umeme wa uhakika na wa bei nafuu. Itakapokamilika miundombinu hiyo **itaokoa zaidi ya Dola za Marekani bilioni moja (\$1bilioni) sawa na Shilingi trilioni 1.6 kwa mwaka zinazotumika sasa kuagiza mafuta kwa ajili ya kufua umeme** kwa kutumia mitambo ambayo tayari ipo nchini. Kadhalika mitambo mipya inayojengwa itapata gesi asilia kuzalisha umeme wa bei nafuu.
- b) **Kupanuka na Kuongezeka kwa Viwanda:** Kukamilika kwa mradi huu kutachochea maendeleo ya viwanda nchini kwani viwanda vingi vimeonesha nia ya kutumia nishati ya gesi asilia katika kuendesha mitambo yake ya uzalishaji. Aidha, umeme wa uhakika utapunguza gharama za uzalishaji na kufanya bidhaa za Tanzania kuuzika katika masoko mbali mbali dunia (*Competitive products*).
- c) **Utunzaji wa Mazingira:** Kukamilika kwa mradi huu kutachochea matumizi ya gesi asilia majumbani na katika shughuli za usafirishaji na hivyo kupunguza uchafuzi wa mazingira, utumiaji wa mkaa na kuni nchini mwetu.
- d) **Upatikanaji wa Ajira:** Kukamilika kwa mradi huu kutachochea upatikanaji wa ajira mpya nyingi nchini kutokana na kuwepo kwa umeme wa uhakika viwandani, mashambani na kwa biashara za aina mbalimbali.
- e) **Matumizi ya Gesi Asilia katika Maeneo Ambayo Bomba la gesi asilia Linapita:** Bomba la kusafirisha gesi asilia limeweka matoleo ya kuchukulia gesi (off take) katika miji ya Mtwara, Lindi, Kilwa na Mkuranga ili kuhakikisha kuwa miji hii inapata gesi asilia ya uhakika ya kupeleka kwenye viwanda vilivyopo na vitakavyojengwa, majumbani, mitambo ya kuzalisha umeme pamoja na mahitaji yoyote ya gesi asilia yatakayojitokeza.
- f) **Maji Safi:** katika mitambo ya kusafishia gesi asilia itakayojengwa Madimba na Songo Songo kutajengwa mitambo ya kusafishia maji na vijiji hivyo vitapatiwa maji safi. Hadi sasa tayari Mkandarasi ameshakamilisha uchimbaji wa visima vitatu vya maji eneo la Madimba vyenye uwezo wa kuzalisha mita za ujazo 150 kwa saa

(150m³/hr). Sehemu ya maji hayo yatatumika katika mtambo wa kusafishia gesi asilia na sehemu nyingine itahudumia wanakijiji.

g) **Nishati Viwandani:** Gesi asilia hutumika kama malighafi katika viwanda mbalimbali kama; mbolea, Kemikali (*Petrochemicals*), Aluminium pamoja na kutengeneza vifaa vya plastic. Uanzishwaji wa viwanda vipya kutokana na matumizi ya gesi asilia kutachochea kukua kwa uchumi wa nchi yetu, na kwa upatikanaji wa ajiri mpya nyingi kwa vijana wetu.

Mradi wa Ujenzi wa Bomba la Gesi Asilia ni Muhimu sana kwa Utekelezaji wa **Dira yetu ya Maendeleo ya Mwaka 2025**. Tanzania imeingia kwenye Uchumi wa Gesi Asilia na Miundombinu ya aina hii ya Uchumi lazima ijengwe. Gharama za Ujenzi wa Bomba letu ni nafuu sana kulinganisha na ujenzi wa Mabomba ya aina hiyo kwingineko duniani.

Taarifa kamili inapatikana pia katika tovuti ya Wizara ya Nishati na Madini (www.mem.go.tz) na TPDC (www.tpdc-tz.com).

Kwa ufafanuzi zaidi wasiliana na:

Mkurugenzi Mtendaji;
Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC)
Benjamini W. Mkapa Pension Tower,
Tower "A", Azikiwe/Jamhuri Street
S.L.P 2774, DAR ES SALAAM, Tanzania
Simu: +255 22 220 0103/4
Nukushi: +255 22 220 0113
Barua Pepe: tpdcmd@tpdc-tz.com
Tovuti: www.tpdc-tz.com